

WATEULE TUNAYE MUNGU AMBAYE NI FUNDI NA BINGWA WA MATENGENEZO.

MAANDIKO: RUMI 8:11; MARK. 5: 25 – 34

1. UTANGULIZI:

Mtume Paulo anapewa ufunuo wa wazi kuwa Roho Mtakatifu ndiye aliyemfufua Yesu Kristo katika wafu na kumfanya atoke akiwa hana vidonda wala makovu ya mijeledi mwilini mwake; na anasema Roho Mtakatifu huyo huyo ndiye **atakayeihusiha** (“Restore to life”) na miili yetu iliyo katika hali ya kufa; ndiye atakayerudisha/atakayetengeneza afya zetu na hata baraka zetu kwa ujumla ambazo zimeharibiwa na ibilisi huko nyuma

- Na leo nataka nitangaze na kutoa tamko kwa watoto wa Mungu wote kwamba hawana sababu ya **kuzimia mioyo na kuweweseka hovyo kutokana na uharibifu wa adui shetani uliotangulia kufanywa katika maisha yao na kazi zao; natangaza hadharani kwamba hakuna uharibifu wa aina yoyote uliotangulia kufanywa na ibilisi katika maisha yako ambao Mungu anashindwa kuutengeneza, tunaye Mungu Mkuu sana ambaye ni fundi na bingwa wa matengenezo yote. Shetani sifa yake kuu ni kuharibu na Mungu sifa yake kuu ni kutengeneza!!**

2. Katika historia nzima ya Biblia Takatifu, shetani kama adui mkubwa wa wana wa Mungu, wakati wote **anatangulia kuharibu** kwa lengo la kumfanya mteule akate tamaa na kuchanganyikiwa kama alivyofanya kwa wana wa Israel.

Kut 1:8-14, 15-22, 2:1-10 (Kwa kadri anavyojitahidi kuharibu ndivyo Mungu wetu anavyokuja na mbinu bora zaidi ya matengenezo kwani hakuna kabisa jambo lolote la mwana wa Mungu ambalo shetani ameliharibu ambalo Roho Mtakatifu anashindwa kulitengeneza. *Rum 8:11.*

- Kama shetani alikuwa na wakati wa kutamba na kufanya sherehe zake, basi ulikuwa ni wakati wa kifo cha Bwana wetu Yesu Kristo pale msalabani, lakini **ghafla bini vuu**, Yesu akatoka kaburini (akafufuka) anazo funguo na mamlaka yote, tambo zote za ibilisi zikazimwa. **Filp 2:9-11** na **Ufun. 1:17-18, Ayub. 20:4-7**
 - Kuna kipindi cha nyuma **aliharibu** kabisa maisha ya Mtumishi wa Mungu Ayubu kwa hila (**Ayub 1:8-20, 2:1-8, 19:12-27**), lakini Mungu ambaye ni fundi na bingwa wa matengenezo alibadili hali ya Ayubu ghafla na historia yake ya mwisho ikawa bora kuliko ya nyuma. **Ayub 42:10-17**
- Yaani:** Pale magonjwa (shetani) yalipoharibu kabisa mwili wa **Lazaro** hadi kufa na kuanza kunuka, ndipo Yesu alipotengeneza upya mwili wa Lazaro na akafufuka kwa utukufu mkuu. **Yoh. 11: 38 – 45.**
- Pale alipodhani kwamba amefaulu **Sara** mkewe Ibrahimu kuitwa tasa na tumbo la uzazi wake kufa; Yesu fundi na bingwa wa matengenezo akashughulika na ndani ya tumbo hilo hilo akakaa Isaka na kisha kuzaliwa!! **Mwanz 21:1-7** na kumfanya Sara acheke kwa furaha ya ajabu mno mbele ya jamii iliyokuwa imembeza
 - Pale alipoharibu heshima ya **Mordekai** na kupanga kumtundika juu ya mti mrefu kesho yake, ndipo Yesu ambaye ni fundi na bingwa wa matengenezo alipobadili mipango hiyo yote ndani ya muda mfupi kabisa. **Esta. 5:9-14, 6:1-12** na badala ya Mordekai kutundikwa, anapitishwa mjini kwa heshima zote
 - Pale alipoharibu maisha ya **binti huyu** kwa magonjwa na kufilisi mali zake na kumfanya azeke haraka sababu ya

kuwaza usiku na mchana bila majibu, ndipo Yesu fundi na bingwa wa matengenezo alipomshughulikia na kumrejesha ubinti wake na furaha yake ya ajabu. **Mark. 5:25-34.**

- Pale anapoharibu uchumi wa wana wa Mungu na kuwafanya wafanye kazi kubwa tena za mchana kutwa na usiku kucha bila kupata faida yoyote, ndipo fundi na bingwa Yesu anapoingilia kati na kuwafanya wapate faida maradufu na kushangaza wengi. **Luk. 5:1-11**

3. Hili ni muhimu sana kwa wateule kulielewa; pale shetani anapomwonea mwana wa Mungu na kumtesa ikiwa ni pamoja na kuharibu **afya yake, kazi yake, uzao wake**; wakati huo huo Yesu anakuwa kama mchezaji fundi anapoonna timu yake imefungwa; anaanza kupasha (anapiga jalamba) mikono yake inaanza kumwasha maana sasa amepata **kazi ya kufanya** na kwa hakika hata hivi ninavyofundisha mbele yenu; Yesu anataka kufanya jambo jipya na la tofauti katikati yetu. Mbele za Mungu ambaye ni fundi na bingwa wa matengenezo historia ya mtu hutengenezwa na kukamilishwa kwa muda mfupi sana na jambo jipya linazaliwa ndani yake na kumfanya ajae kicheko. **Isaya 43: 18-20; Natangaza ole leo kwa ibilisi-Isay. 33:1**

- **Zab 30:11**; Zaburi hii ya 30 iliandikwa na Mfalme Daudi ambaye alipitia katika kipindi kirefu cha mateso na kuvaa magunia akiomboleza, lakini ghafla bini vuu Bwana alimvua gunia na akamvika furaha ya ajabu!! Anataka afanye hivyo hata sasa, yeye ni fundi na bingwa wa matengenezo; anataka atuvike furaha na kutuvua gunia la maombolezo ya nyuma; Yesu ni yule yule jana, leo na hata milele. **Ebr 13:8. Amina**

Na

Askofu Dr L. M. Mwizarubi

April- 2022

